

“TUMEJIPANGA KUPOKEA NA KUTOA MAJIBU YA MAOMBI YA UHAKIKI KWA WAKATI”



Mkurugenzi Mtendaji wa Bodi ya Mikopo Abdul-razaq Badru akitoa ufafanuzi kuhusu kuanza rasmi kupokea maombi ya mikopo ya elimu ya juu hii leo jijini Dar es salaam, wa kwanza kushoto kwake ni Mwenyekiti wa Shirikisho la Serikali za wanafunzi wa Vyuu Vikuu (TAHLISO) George Mnali, kulia kwake ni Kaimu Mkuu wa Shirika la Posta Tanzania Hassan Mwangombe mwingine ni Kaimu Meneja wa Usajili wa Vizazi na Vifo Patricia Mpuya.

Wanafunzi wote wanaotarajia kuomba mikopo kutoka Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu (HESLB) wametakiwa kuanza mapema hatua za maombi ikiwemo nyaraka za uthibitisho kwa watendaji wa mitaa, vijiji, Kata, Mahakama na wanasheria pamoja na kuhakiki vyeti vya kuzaliwa au vifo vya wazazi wao kwa njia ya mtandao iliyowekwa na Wakala wa Usajili Ufilisi na Udhadini (RITA).

Hayo yamezungumzwa na Mkurugenzi Mtendaji wa Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu Abdul-razaq Badru hii leo jijini Dar es salaam wakati wa ufunguzi rasmi wa kupokea maombi ya mikopo ya elimu juu na kuwataka wanafunzi wasisubiri tarehe za mwisho wa kupokea maombi ndipo waanze hatua za maombi jambo linalochangia kuleta usumbufu kila mwaka.

Wanafunzi wapya zaidi ya 40,000 na wanaoendelea na masomo wapatao 80,000 kwa mwaka wa masomo 2018/2019 watapatiwa mikopo ambapo zaidi ya shilingi bilioni 427 zimetengwa kwa ajili hiyo na kwamba wanafunzi wasiwe na hofu wahakikishe wanakamilisha kwa usahihi ujazaji wa fomu pamoja na nyaraka muhimu zinazohitajika kuanzia leo tarehe 10 Mei hadi julai 15 mwaka huu.

Ameendelea kusema kuwa mwaka huu ni tofauti na miaka mingine kutokana na maboresho ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) kwa wadau wote kuanzia

uhakiki wa cheti cha kuzaliwa na vifo unaofanywa na RITA na kwa upande wa shirika la Posta Tanzania katika hatua ya utumaji wa fomu za maombi ya mikopo.

“Tumeshirikiana na Taasisi zote zitakazohusika katika uhakiki wa nyaraka hivyo kazi itakuwa rahisi ukilinganisha na miaka mingine na leo kwa pamoja mnawaona hapa RITA, Shirika la Posta na Shirikisho la Serikali za wanafunzi wa Vyuo Vikuu (TAHLISO).” Alisema Badru.

Kwa upande wake Kaimu Meneja wa Usajili wa Vizazi na Vifo Patricia Mpuya amesema kuwa RITA imeshaanza kupokea maombi ya uhakiki kupitia mtandao ambapo mwanafunzi ataweza kutuma maombi yake na kujibiwa ndani ya siku tatu.

Ameendelea kusema kuwa Mwaka huu kumetengenezwa ukurasa maalum (portal) ambayo ni <http://uhakiki.rita.go.tz/uhakiki>, ambapo kila anayehitaji kuhakiki cheti atatakiwa kujisajili katika ukurasa huo na kupewa akaunti maalumu ambayo ataitumia kuambatanisha cheti na stakabadhi ya malipo ya ada na kutuma RITA na baada ya uhakiki atapokea majibu kupitia akaunti hiyo.

“Tunasisitiza matumizi ya mtandao, pia mwanafunzi anatakiwa kulipia ada ya Uhakiki kwa kila cheti TShs. 3,000/= (elfu tatu) na ilipwe kupitia Benki ya NMB kwenye akaunti ya Administrator General Collection Account Na. 20610009881 au Benki ya CRDB kwenye akaunti ya Administrator General Collection Account Na. 0150339892600 kisha utatuma nakala ya cheti na risiti ya malipo kwa njia hiyo ya mtandao.” alisema Mpuya.

Kwa upande wake Kaimu Mkuu wa Shirika la Posta Tanzania Hassan Mwangombe amesema wameweka vituo 177 Nchi nzima vya intaneti (Internet Cafe) kwa ajili ya kuwasaidia Wanafunzi watakaomba Mikopo ya Elimu ya Juu hivyo ni muhimu kutembelea katika ofisi za Posta zilizopo katika kila wilaya badala ya kwenda mitaani ambapo wengi wao wamekuwa wakitapeliwa na kushindwa kutuma maombi kwa wakati.

“tutahakikisha mwaka huu tunatoa msaada na huduma stahiki kwa Wanafunzi wote watakaomba mikopo kutumia njia za mtandao kuhakiki vyeti na kutuma maombi yao Bodi ya Mikopo”.

Naye Mwenyekiti wa Shirikisho la Serikali za wanafunzi wa Vyuo Vikuu (TAHLISO) George Mnali ameahidi kufikisha taarifa katika vyuo vyote vikuu ili kuwahimiza wanafunzi kutumia ipasavyo muda waliopewa kufanya uhakiki na kutuma maombi yao kwa wakati.

“ Tayari nimeshafanya mazungumzo na RITA na kwa upande wao wamenihakikishia kuwa mwaka huu wamejipanga vizuri zaidi kutoa majibu kwa wakati hivyo sina wasiwasi juu ya hilo.” Alisema Mnali.